**JAMHURI YA MUUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA**

SHULE YA SEKONDARI NYAMAGANA
S.L.P 4057, MWANZA
TAREHE………………….

**MZAZI/MLEZI WA**
**MWANAFUNZI…………………………………………………………….WA**
**S.L.P…………………………………**

**YAH; MAELEKEZO MUHIMU YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA ……………… SHULE YA SEKONDARI NYAMAGANA.**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano kwa mwaka wa masomo ……………….. Shule ipo kata ya Butimba, mtaa wa Iseni karibu na Shule ya Msingi Iseni,wilaya ya Nyamagana mkoa wa Mwanza.

**1. USAFIRI**

Ufikapo mjini Mwanza; kama umeshuka kituo cha mabasi cha Nyamongolo panda daladala ziendazo Buhongwa na ushukie Iseni. Kisha panda Pikipiki kuja shule ya sekondari Nyamagana .Nauli ya pikipiki ni tsh.1000.

Au kwa atayeshukia kituo cha mabasi cha Nyegezi (Nyegezi Bus Terminal) apande daladala ziendazo mjini na ashuke Iseni. Kisha panda pikipiki kuja shule ya sekondari nyamagana.Nauli ni tsh.1000.

Au atakayekuja na usafiri wa anga apande daladala ziendanzo Airport – Buhongwa na ashukie Iseni. Kisha panda pikipiki kuja shuleni. Nauli ni Tshs.1000.

Muhula wa masomo unaanza tarehe …………………….. Hivyo, mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ……………………. Mwisho wa kuripoti ni tarehe …………………... Muda wa kuripoti mwisho ni saa 11 jioni baada ya hapo hautapokelewa.

**MAELEKEZO KWA WANAFUNZI**

**SARE YA SHULE**

**a)** Shati mbili Tretoni Nyeupe zenye mikono mirefu ambazo hazibani mwili na ziwe na mfuko mmoja upande wa kushoto zinazovaliwa kwa kuchomekea pia ziwe na ufito (bar) kulia begani kuonesha kidato anachosoma.

**b)** Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi vya kufunga na Kamba vyenye visigino vifupi, vinavyofunika miguu na visivyo na uwazi na vinavyosafishwa kwa kiwi nyeusi. Boots na viatu vinginevyo havitakiwi kabisa.

**c)** Sweta moja rangi ya Dark Blue

**d)** T-shirt ya rangi ya Light Blue yenye ukosi mweusi na mfuko upande wa kushoto

**e)** Track suit moja ya rangi ya Dark Blue yenye fito tatu nyeupe mabegani (Ni marufuku kubana suruali ya Track)

**f)** Nembo ya shule

*g)* Sketi mbili ndefu hadi kwenye kifundo cha mguu (mshono wa Marinda 16) usiache nafasi kwenye fundo la mguu kupanda juu. Rangi ya sketi ni Blue green kitambaa cha suti. Aidha kwa wanafunzi wa kiislamu watavaa nusu kanzu nyeupe na juba (hijab) nyeupe ndefu kitambaa cha tetron na kilemba cha ndani kiwe rangi ya Blue Green.

*h)* Soksi jozi mbili Nyeupe ndefu.

*i)* Raba nyeupe kwa ajili ya michezo.

*j)* Magauni mawili (02) marefu ya kushindia rangi ya bluu sister moja na pink sister moja (shamba dress)

k) Tai 02 zenye mistari zenye logo ya shule, zinapatikana shuleni

***MUHIMU;*** Masweta, Fulana na Mashati ni lazima yawe na nembo ya shule. (Utapewa maelekezo shuleni).

**MAHITAJI BINAFSI**

- Vyombo vya chakula: (sahani, bakuli, kijiko, Chupa ya maji ya kunywa na kikombe (viwe vya mfupa, Vyombo vya plastic haviruhusiwi).

- Vifaa vya darasani: (mathematical set, counter book 3quire, art na biashara yasipungue 10 na sayansi yasipungue 12 kalamu za kutosha, ruler, penseli). Vile vile aje na madaftali ya kawaida 05 kwa ajili ya mazoezi ya darasani
- Aje na Taa ya Solar isiyo na mwanga hafifu kwa tahadhali.
- Mahitaji binafsi: (sabuni za kuogea na kufulia, taulo, khanga au kitenge pair 1, soap dish, vibanio ya nguo,kandambili pair moja,mafuta ya kupaka,dawa ya meno na miswaki,toilet paper, night dress na nguo za ndani za kutosha)
- Kamba ya kuanikia nguo
- Godoro, Neti nyeupe, Ndoo ndogo, na Blanketi
- Trunker moja(sanduku bati) la kuhifadhia vitu na makufuli yake.
- Mashuka mawili: moja rangi ya blue bahari na moja rangi ya pink.

**MAHITAJI YA DARASANI.**

a) Madaftari makubwa 9 **(**Counter book Quire 3 au 4**).** Madaftari 8 madogo ya msomi kwa ajili ya mazoezi.

b) Mkebe (Mathematical set), kalamu na rula.

c) Begi la shule la kubeba madaftari la mgongoni (School bag). Mikoba au mifuko isiyo rasmi hairuhusiwi

d) Scientific calculator (Casio Fx 991 MS) au Casio FX991 ES original

e) Faili mbili (Spring file) kwa ajili ya kutunzia taarifa muhimu za wanafunzi (Faili moja ije ikiwa imewekwa fomu ya kujiunga iliyojazwa).

f) Nakala ya cheti cha kuzaliwa

g) Rim paper 02- Double A

h) Ufagio wa chelewa wa nje wenye mpini

i) Picha 2 passport size

j) Mwanafunzi anashauriwa kujiunga na bima ya Afya ya Taifa (NHIF) kwa kuchangia shilingi 50,400/- kwa mwaka kwa wanafunzi wasiokuwa na Bima ya Afya.

k) Kitambulisho cha Shule

l) Graph pad mbili kwa masomo ya Sayansi, na wale wanaosoma somo la Jografia. GRAPH PAD Moja atabaki nayo mwanafunzi na Moja atakabidhi shuleni.

m) **Dissecting kit** kwa wanafunzi wa “**biology”.**

n) Vitabu vya masomo ya tahasusi (Combination) husika.

**VIFAA VYA USAFI**

**(i).** Fyekeo

**(ii).** Ndoo ndogo moja

(iii) Mopper moja

(iv)Soft broom moja

**(v) Toilet brush moja na kopo lake**

**(vi)Hard broom moja**

**NB: Mahitaji tajwa hapo juu unaweza kuyapata shuleni.**

**MICHANGO INAYOTAKIWA KULIPWA NA KILA MZAZI NI:**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Tanbihi:** Fedha yote ya michango ilipwe katika Benki ya NMB; Jina la Akaunti ni **Nyamagana Secondary School – School Fund, Account No. 31101200145.**

**WAJIBU WA MZAZI/MLEZI KATIKA ELIMU**

Waraka wa Elimu wa Mwaka 2015 unaelekeza majukumu ya mzazi/mlezi katika usimamizi wa elimu kama ifuatavyo;

a) Kuhakikisha kuwa mwanao anahudhuria masomo shuleni kwa siku zote za masomo bila kukosa.
b) Kumpatia mwanafunzi mahitaji muhimu ya shule kama sare, madaftari, vitabu, kalamu na nauli ya kurudi nyumbani
c) Kushirikiana na uongozi wa shule kufuatilia taaluma ya mwanao na kuhudhuria vikao vya shule mara anapohitajika kufanya hivyo.

d) Kushirikiana na wazazi wenzako pamoja na wadau wengine wa elimu katika kuboresha taaluma na miundombinu ya shule na kutatua changamoto mbalimbali kwa ustawi na maendeleo ya elimu.

e) Jukumu la matibabu ni la mzazi/ mlezi unashauriwa kumfungulia mwanao bima ya afya akiwa nyumbani**. Kwa ambae hana bima ya afya aje na tshs 50,400/= atalipia akiwa shuleni (pesa hii isiwekwe kwenye akaunti ya shule mwanafunzi aje nayo mkononi)**

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

- Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
- Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
- Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- Kuvaa sare ya shule wakati wote kulingana na taratibu za shule.
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
- Kutunza mali za shule;
- Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
- Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
- Mwanafunzi haruhusiwi kujihusisha na biashara yoyote awapo shuleni

**MUHIMU:-**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu na viambata vyake shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

- Wizi;
- Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
- Kugoma na kuhamasisha mgomo;
- Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
- Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
- Kusuka nywele (Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni).
- Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
- Uvutaji wa sigara;
- Uasherati, mahusiano ya jinsia moja, kuoa au kuolewa;
- Kupata ujauzito au kutoa mimba;
- Kusababisha mimba;
- Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
- Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
- Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
- Kudharau Bendera ya Taifa;
- Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
- Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatanisho na fomu Muhimu**

- Fomu ya uchunguzi wa Afya (Medical Examination form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospital ya Serikali.
- Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
- Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule, na
- Picha nne za Wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi watakao wajibika wakati wote mwanafunzi awapo shuleni pamoja na namba za simu.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekele kikamilifu.**

**Tanbihi:** Mwanafunzi anapokuja kuripoti shuleni aje na :-

- Cheti cha kuzaliwa (photocopy siyo original)
- Result slip (photocopy siyo original) ya kidato cha nne.

Nakutakia maandalizi mema.

Karibu Shule ya Sekondari Nyamagana

………………..

Mwl.Malima P.Chisumo.

MKUU WA SHULE. 0754 697147

MAKAMU UTAWALA; 0743 624720

MAKAMU NIDHAMU/ MALEZI: 0613111241

## FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA

*(MEDICAL EXAMINATION FORM)*

- **MUHIMU:** *ijazwe na Mganga mkuu wa Hospitali ya Wilaya*

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF A STUDENT SELECTED TO JOIN FORM ONE 2025.

**NAME OF THE STUDENT,**

**……………………………………………………………………………………**

Please examine the mentioned as to his/her fitness for Secondary School education according to the items below;

| No. | ITEM | CONDITION | REMARKS |
|---|---|---|---|
| 1 | **Mental condition** | | |
| 2 | **Sight** | | |
| 3 | **Hearing** | | |
| 4 | **Chest TB** | | |
| 5 | **Urine** | | |
| 6 | **Stool** | | |
| 7 | **Nose** | | |
| 8 | **Blood BP, HB** | | |
| 9 | **Pregnancy test** | | |

**Any other physical disability not listed that may affect his/her studies**

**…………………………………**

**………………………………………………………………………………………………………**

**………………………………………………………………………………………………………**

**……………………………………**

**In my opinion the student is fit/unfit to join Secondary School Education**

**………………………………………………………………………………………………………**

**………………………………………………………………………………………………………**

**……………………………………**

**Signed ……………………………….**

**Medical officer ……………………………………**

**Stump ……………………………**

**FOMU YA KURIPOTI SHULENI**

**SHULE YA SEKONDARI NYAMAGANA**

- Tarehe ya kuingia Shuleni ................................ Admission No. ...........................
- Jina la Mwanafunzi ..........................................................................................
- Darasa na mchepuo anaoingia ...........................................................................
- Kabila ..................................................................................................................
- Tarehe ya kuzaliwa .............................................. Wilaya ..................................
- Jina la baba/mlezi ..............................................................................................
- Kazi ya baba/mlezi ............................................................................................
- Namba ya simu ya baba/mlezi ...........................................................................
- Mahali baba/mlezi anapoishi ..............................................................................

**HISTORIA YA MWANAFUNZI**

- Jina la Mwanafunzi ................................................Mchepuo....................
- Dini/madhehebu .................................................................................
- Michezo aipendayo au hobby. ...................................................................

Picha

(a) **Taarifa za Baba**

- Jina la Baba…….. ....................................................(HAI/AMEFARIKI)
- Dini/madhehebu ..............................................................................
- Kazi ya baba ……………….. .....................................................................

Picha

Mahali baba anaishi

- Kijiji .......................................... Wilaya ................................ Anwani yake .......................... Namba yake ya Simu ...................................................

(b) **Taarifa za Mama**

Picha

- Jina la Mama……... ........................................................(HAI/AMEFARIKI)
- Dini/madhehebu ......................................................................................
- Kazi ya mama ……………… ......................................................................

Mahali baba anaishi

- Kijiji .................................................. Wilaya ..................................... Anwani yake...................................... Namba yake ya Simu ............................................

**Taarifa za Mlezi anayehusika na taarifa za mwanafunzi**

**Awapo shuleni**

Picha

- Jina la Mlezi…….. ..........................................................................................
- Uhusiano …………………………………………………………………
- Dini/madhehebu ..........................................................................................
- Kazi ya Mlezi ………………..........................................................................

Mahali Mlezi anaishi

- Kijiji ........................................................................................... Wilaya
  ...................................... Anwani yake ..................................................................
  Namba yake ya Simu ..........................................................................................
- Tatizo la kiafya kwa mwanafunzi (lipo/halipo) kama lipo
  eleza:..........................................................................................................................
  ..................................................................................................................................
  ..................................................................................................................................
  ..................................................................................................................................
  ..................................................................................................................................
  ..........................................................................
- Taja ndugu wanne watakaowajibika kwa mwanafunzi shuleni:
  - .......................................................................... simu ....................................
  - ................................................................... simu ..........................................
  - .......................................................................... simu ....................................
  - ........................................................................ simu ....................................

Jina la mwanafunzi ............................................................ sahihi yake ....................

Darasa na tahasusi anayosoma ......................................................................................

## MAELEZO YAKE KUHUSU TAALUMA

- Malengo yangu katika kufaulu mitihani ya masomo nitakayochukua ni:

| MASOMO | ALAMA/GRADE |
| --- | --- |
| • ........................................................................ | ........................................ |
| • ..................................................................... | ........................................ |
| • ................................................................... | ........................................ |
| • ......................................................................... | ........................................ |
| • ......................................................................... | ........................................ |

- Mikakati yangu ili kufikia malengo hayo:
  - ..............................................................................................................................
  - ..............................................................................................................................
  - ..............................................................................................................................
  - ..............................................................................................................................
  - ..............................................................................................................................

- Nikishindwa kufikia malengo yangu nini kifanyike?

.........................................................................................................................................
.........................................................................................................................................
..............................................................................................................

## MWANAFUNZI KUKIRI KUZIFUATA SHERIA NA TARATIBU ZOTE ZA SHULE

Mimi ............................................................................................ wa kidato cha tano .................... tahasusi ya ................................. nimezisoma na kuzielewa, na kuzikubali sheria, kanuni na taratibu zote za shule kama zilivyoorodheshwa hapo juu.

..............................................

**SAHIHI YA MWANAFUNZI**

**AHADI YA MZAZI**

Mimi mzazi/mlezi wa .......................................................................................... na ahidi kumhimiza mtoto wangu kusoma kwa bidii, kulipa michango yote ya shule na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule ikiwa ni pamoja na kuhudhuria vikao vya wazazi shuleni na kufuatilia maendeleo yake ya taaluma.

**Jina la mzazi/mlezi ........................................ sahihi ya mzazi/mlezi ..................**